GAZETI LA SERIKALI Na. 631 la Tarehe13/08/2021

SHERIA YA UMEME
(SURA YA 131)

# KANUNI

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya 8(3), 45 na 46)*

KANUNI ZA UMEME (HUDUMA ZAUFUNGAJI MIFUMO YA UMEME) ZA MWAKA, 2019

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kifungu Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
TARATIBU ZA KUOMBA LESENI

4. Wajibu wa kuomba leseni.
5. Utaratibu wa kuomba leseni.
6. Aina za leseni za ufungaji mifumoya umeme.
7. Sifa za zakupata leseni.
8. Tathimini ya maombi.
9. Utoaji wa leseni.
10. Kukataliwa leseni.
11. Uhalali, muda na uhamishaji wa leseni.
12. Upandishaji daraja na uhuishaji leseni.
13. Usitishaji na ufutajileseni.
14. Kurudisha leseni baada ya kusimamishwa kwa muda au kufutwa.

SEHEMU YATATU
WAJIBU WA MMILIKI LESENI

15.Kazi ya ufungaji mifumo ya umeme.
16.Uzingatiaji wa sheria.
17.Ukaguzi na majaribio.
18.Ajali wakati waufungaji mifumo ya umeme.
19.Wajibu wa mmiliki au mkazi katika jengo.

21. Adhabu ya jumla
SEHEMU YA NNE
WAJIBU WA JUMLA
20. Makosa.

22.Adhabu kwa kuendelea kutenda kosa.
23.Utoaji taarifa ya Makosa.
24.Kukataa kusaini Taarifa ya Makosa.
25.Mamlaka ya kusimamia nataratibu za ziada.
26.Haki ya kukata rufaa.
27.Kufutwa kwa Gazeti la Serikali.

SHERIA YA UMEME
(SURA YA 131)

---

# KANUNI

---

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya8 (3), 45na46)*

---

KANUNI ZA UMEME (HUDUMA ZA UFUNGAJI MIFUMO YA UMEME) ZA MWAKA 2019

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji Mifumo ya Umeme) za Mwaka 2019.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika masuala ya usimamizi na utoaji wa leseni ya hudumaza ufungaji mifumo ya umeme Tanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 131

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Umeme;

"sheria itakayotumika" maana yake ni sheria yoyote, mkataba wa kimataifa, tangazo, kanuni, amri au sheria ndogo ambayo inatumika Tanzania na yenye nguvu kisheria kuhusu usimamizi wa huduma za ufungaji mifumo ya umeme;

Sura ya 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ambayo imeanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji;

"shughuli za ufungaji wa mifumo ya umeme" maana yake ni shughuli inayohusukuunganisha vifaa mbalimbali vya umeme ili kuvileta pamoja kwenye mfumo unaoweza kuunganishwa kwenye chanzo kimoja kwa ajili ya kutekeleza madhumuni

maalum na kuwa na sifa zinazoendana;

Sura ya 414

"Sheria ya EWURA" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma zaNishati na Maji;

"FTC"maana yake ni Cheti cha Ufundi sanifu;

"msongo mkubwa"maana yake ni mkondo wowote wa umeme wenye msongo wa zaidi ya volti elfu thelathini na tatu au pungufu kwa asilimia kumi ya kiwango husika;

"kV" maana yake ni kilovolti;

"leseni"maana yake ni leseni ya ufungaji mifumo ya umeme inayotolewa na Mamlaka chini ya Kanuni hizi;

"mmiliki leseni" maana yake ni mtu mwenye dhamana ya umiliki wa leseni;

"wataalam wa ujenzi wa njia za umeme" maana yake ni watu wenye taaluma ya ujenzi na matengenezo ya vituo vya kupooza umeme na njia za kusafirisha na kusambaza umeme;

"msongo mdogo" maana yake ni mkondo wowote wa umeme wenye msongo ambao ni chini au sawa na volti elfu moja zaidi au pungufu kwaasilimia tano ya kiwango husika;

"msongo wa kati" maana yake ni mkondo wa umeme wenye msongo ambao ni zaidi ya volti elfu moja na usiozidi au pungufu ya volti elfu thelathini na tatu zaidi au pungufu kwa asilimia kumi ya kiwango husika;

Sura ya 130

"Viwango vya Kitaifa" maana yake ni viwango vinavyofanyika chini ya Sheria ya Viwango Tanzania;

"NTAL" maana yake ni Ngazi ya Tuzo ya Kiufundi ya Kitaifa;

"kazi maalum za ufungaji wa mifumo ya umeme" maana yake ni kazi ambazo zinatakiwa kufanywa na mtu mwenye ujuzi maalum katika eneo fulani la uhandisi wa umeme na uzoefu wa kutosha wa vitendo ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwenye njia za umeme bila kuzima umeme, kusuka mota, kuunganisha nyaya, nishati jadidifu, mtaalam wa kujenga njia za umeme na vituo vya kupooza

umeme na utengenezaji wa mifumo ya umeme wa vifaa vya maabara za tiba na hospitali.

## SEHEMU YA PILI
## TARATIBU ZA KUOMBA LESENI

Wajibu wa kuomba leseni

4.-(1) Mtu hataruhusiwa kufanya shughuli za kufunga mifumo ya umeme bila kuomba na kupata leseni inayotolewa na Mamlaka.

(2) Mtu ambaye amekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) atatakiwa kulipa faini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Utaratibu wa kuomba leseni

5.-(1) Kama ilivyoelekezwa katika kanuni ndogo ya (2), mtu atafanya maombi ya leseni ya kufunga mifumo ya umeme kupitia fomu na kwa namna ilivyoainishwa katika tovuti ya Mamlaka.

(2) Maombi ya leseni yataambatana na-

(a) nakala za vyeti vya elimu yamwombaji vilivyothibitishwa;

(b) wasifu wa mwombaji i katika muundo ulioainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(c) picha ya passipoti ya rangi iliyopigwa karibuni;

(d) kibali cha kufanya kazi kwa mwombaji ambaye siyo raia; na

(e) ada ya maombi ambayo haitarudishwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni ya 2(a), cheti kilichotolewa na taasisi ya kigeni kitathibitishwa na mamlaka husika ya Tanzania.

Aina za leseni za ufungaji wa mifumo ya umeme

6.-(1) Yafuatayo ni madaraja ya leseni zinazotolewa na Mamlaka-

(a) Daraja A: inatolewa ili kuweza kufanya kazi za ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa umeme wa aina zote;

(b) Daraja B: inatolewa ili kuweza kufanya kazi za ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa kati mpaka kiasi cha msongo wa volti 33,000;
(c) Daraja C: inatolewa ili kuweza kufanya kazi za ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa umeme usiyozidi volti 400;
(d) Daraja D: inatolewa ili kuweza kufanya kazi za ufungaji mifumo ya umeme usiyozidi volti 220;
(e) Daraja W: inatolewa ili kuweza kufanya kazi za ufungaji mifumo ya umeme chini ya usimamizi wa mwenye leseni Daraja A,B,C au D;
(f) Daraja “S1”: inatolewa ili kufanya kazi maalum za ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa aina zote;
(g) Daraja “S2”: inatolewa ili kufanya kazi maalum za ufungaji mifumo ya umeme mpaka msongo wa volti 33,000; n a
(h) Daraja S3: inatolewa ili kufanya kazi maalum za ufungaji mifumo ya umeme mpaka msongo wa volti 1,000.

(2) Bila kujali mipaka ya kazi iliyoainishwa, mmiliki wa leseni daraja A, B, C na D hataruhusiwa kufanya kazi yoyote iliyo chini ya leseni maalum pasipo kuwa na leseni husika.

Sifa zinazohitajika ili kupata leseni

7.-(1) Mtu hatapewa leseni ya ufungaji mifumo ya umeme mpaka mtu huyo:

(a) ikiwa ni leseni Daraja “A”, atatakiwa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo-
(i) cheti cha Usajili cha Utaalam wa Uhandisi wa Umeme na vyeti husika vya elimu;
(ii) shahada ya uhandisi wa umeme au uhandisi Umeme-Mitambo au Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi ngazi ya 8 au zaidi na miaka minne ya uzoefu katika

masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme, miaka miwili kati ya hiyo iwe ya ufungaji wa mifumo ya umeme kwenye msongo wa juu;

(iii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 7 au Stashahada ya Juu ya Uhandisi wa Umeme na miaka mitano ya uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme, miaka mitatu kati ya hiyo iwe ya ufungaji umeme katika msongo wa juu;

(iv) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 6 au Cheti cha Ufundi sanifu katika masuala ya uhandisi wa umeme na miaka saba ya uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme, minne kati ya hiyo iwe ya ufungaji mifumo ya umeme wa msongo wajuu;

(b) ikiwa ni leseni Daraja "B" anapaswa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo-

(i) shahada ya Uhandisi wa umeme au uhandisi wa Umeme-Mitambo au Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 8 au zaidi na miaka mitatu ya uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme, miaka miwili kati ya hiyo iwe ya ufungaji wa umeme katika msongo wa kati;

(ii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 7 au Stashahada ya Juu ya Uhandisi wa Umeme na miaka minne ya uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme, mwaka mmoja na nusu kati ya hiyo iwe ya ufungaji umeme wa msongo wa kati;

(iii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi

Ngazi ya 6 au Cheti cha Ufundi sanifu katika masuala ya uhandisi wa umeme na miaka sita ya uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme, miaka mitatu kati ya hiyo iwe ya ufungaji wa umeme wa msongowa kati;

(c) ikiwa ni leseni Daraja “C” anapaswa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo-

(i) shahada ya uhandisi wa umeme au uhandisi wa Umeme-Mitambo au Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi ngazi ya 8 au inayolingana na Shahada ya Uhandisi wa Umeme;

(ii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 7 au Stashahada ya Juu ya Uhandisi wa Umeme au inayolingana na hiyo, na mwaka mmoja wa uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme;

(iii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi ngazi ya 6 au ‘Stashahada ya Kawaida ya Uhandisi wa Umeme’ au ‘Cheti cha Ufundi sanifu’katika masuala ya Uhandisi Umeme, au inayolingana na hiyo, na miaka miwili ya uzoefu wa kazi za kufunga mifumo ya umeme;

(iv) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi ngazi ya 4, Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi ngazi ya 5, au Cheti cha kufuzu Mtihani wa ujuzi wa umeme Daraja la Kwanza au inayolingana na hiyo, na miaka minne ya uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya

umeme;

(v) Cheti cha kufuzu cha Mtihani wa ujuzi wa umeme Daraja la Pili au kinacholingana na hicho, na miaka sita ya uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme.

(d) ikiwa ni leseni Daraja “D” anapaswa kuwa namojawapo ya sifa zifuatazo-

(i) Tuzo ya kitaifa ya Kiufundi daraja la 7 au zaidi au stashahada ya juu, Tuzo ya Kitaifa ya Ufundi Ngazi ya 6 au Cheti cha Ufundi sanifu wa umeme;

(ii) Tuzo ya kitaifa ya Kiufundi ngazi ya 4, Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi ngazi ya 5, au Cheti cha kufuzu Mtihani wa ujuzi wa umeme Daraja la I au II au inayolingana na hiyo, na mwaka mmoja wa uzoefu katika masuala ya kazi za kufunga mifumo ya umeme;

(iii) Cheti cha kufuzu Mtihani wa ujuzi wa umeme Daraja la III au inayolingana na hiyo, na miaka mitatu ya uzoefu wa kazi za kufunga mifumo ya umeme;

(e) ikiwa ni leseni Daraja “S1” anapaswa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo:

(i) Cheti cha Usajili cha Utaalam wa Uhandisi wa Umeme na miaka mitatu ya uzoefu wa kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme, mwaka mmoja kati ya hiyo iwe ni kufunga mifumo ya umeme katika msongo wa juu;

(ii) Shahada ya Uhandisi wa Umeme au Uhandisi wa

Umeme- Mitambo au Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 8 na miaka minne ya uzoefu wa kazi za ufungaji mifumo ya umeme miaka miwili kati ya hiyo iwe ni ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa juu wa umeme;;

(iii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 7 au Stashahada ya Juu ya Uhandisi wa Umeme na miaka mitano ya uzoefu wa kazi katika masuala ya kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme, miaka mitatu kati ya hiyo iwe ya ufungaji mifumo ya msongo wa juu;

(iv) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 6 au ‘Cheti cha Ufundi Sanifu’katika masuala ya uhandisi wa umeme na miaka saba ya uzoefu wa kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme, miaka minne kati ya hiyo iwe ya ufungaji umeme wa msongo wa juu;

(f) ikiwa ni leseni Daraja “S2” anapaswa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo:

(i) Cheti cha Usajili cha Utaalam wa Uhandisi wa Umeme na miaka mitatu ya uzoefu wa kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme, mwaka mmoja kati ya hiyo iwe ni kufunga mifumo ya umeme katika msongo wa kati;

(ii) Shahada ya Uhandisi wa umeme au uhandisi wa Umeme-Mitambo au Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 8 na miaka mitatu ya uzoefu wa kazi

maalum za kufunga mifumo ya umeme, miaka miwili kati ya hiyo iwe ya ufungaji umeme katika msongo waKati;

(iii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 7 na zaidi au Stashahada ya Juu ya Uhandisi wa Umeme na miaka minne ya uzoefu wa kazi katika masuala ya kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme, mwaka mmoja na nusu kati ya hiyo iwe ya ufungaji umeme katika msongo wa kati;

(g) ikiwa ni leseni ya Daraja "S3" anapaswa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo:

(i) Shahada ya Uhandisi wa Umeme au uhandisi wa umeme-mitambo au Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundingazi ya 8 na zaidi au inayolingana na Shahada ya Uhandisi Umeme,na mwaka mmoja wa uzoefu wa kazi katika masuala ya kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme;

(ii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 7 au Stashahada ya Juu ya Uhandisi wa Umeme au inayolingana na hiyo, na miaka miwili ya uzoefu wa kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme;

(iii) Tuzo ya Kitaifa ya Kiufundi Ngazi ya 6 au Stashahada ya Kawaida ya Uhandisi wa Umeme au Cheti cha Ufundi Kamili katika masuala ya uhandisi wa umeme au inayolingana na hiyo, na miaka mitatu ya uzoefu wa kazi

maalum za kufunga mifumo ya umeme;

(iv) Tuzo ya Kitaifa ya Ufundi Ngazi ya 4 au cheti cha kufuzu Mtihani wa Ujuzi wa Umeme Daraja la I, II au inayolingana na hiyo, na miaka minne ya uzoefu wa kazi maalum za kufunga mifumo ya umeme.

(h) ikiwa ni leseni Daraja "W" anapaswa kuwa na aidha cheti cha kufuzu Mtihani wa Ujuzi wa Umeme Daraja la I, II au III au vyeti vinavyolingana na hivyo, Cheti ya kufuzu mafunzo ya awali ya umeme, kozi fupi, kozi ya kati, cheti cha juu, au sifa nyingine za kuunganisha mifumo ya umeme kutoka taasisi za ufundi umeme zinazotambulika.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) Mamlaka inaweza, kwa kutumia viwango ambavyo ni sawa na sifa zilizoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), kutoa leseni kwa muombaji ikiwa sifa zake za kitaaluma zitathibitishwa na taasisi ya elimu inayotambulika na leseni itatolewa katika daraja linaloshabihiana na sifa zilizothibitishwa:

Isipokuwa kwamba, muombaji atapaswa kukidhi masharti mengine ya leseni kama Mamlaka itakavyoainisha.

(3) Pamoja na nyongeza ya masharti yaliyoainishwa katika Kanuni hizi na kwa uamuzi wa Mamlaka, muombaji wa leseni anaweza kutakiwa kufanya usaili kwa njia ya maneno au vitendo au vyote kwa pamoja, ambao utafanywa na Mamlaka.

Tathimini ya maombi

8.-(1) Mamlaka itaunda kamati ya kutathimini maombi yote na kuhakiki ukamilifu na usahihi wa taarifa uliopo na kutoa mapendekezo kwenye Bodi kwa ajili ya uamuzi.

(2) Kamati iliyoundwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itajumuisha wajumbe wafuatao:

(a) Meneja Ufundi wa Mamlaka anayehusika na masuala ya leseni ambaye atakuwa

Mwenyekiti;

(b) Meneja Sheria wa Mamlaka ambaye anahusika na Leseni na Utekelezaji wa sheria;
(c) Mhandisi Mkuu mmoja wa Mamlaka anayehusika na masuala ya leseni;
(d) Afisa mmoja kutoka Idara ya Sheria ya Mamlaka ambaye anahusika na masuala ya leseni;
(e) mjumbe mmoja kutoka taasisi ya mafunzo; na
(f) mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na masuala ya umeme.

(3) Kamati itahudumiwa na Sekretariati ikimjumuisha Mkaguzi Mwandamizi wa Umeme na Afisa Leseni Msaidizi, wote kutoka katika Mamlaka.

(4) Baada ya kupokea maombi yaliyokamilika, kamati itatathmini maombi hayo na kutoa mapendekezo yake kwa Mamlaka kwa ajili ya uamuzi.

(5) Kamati itafanya mikutano kwa ajili ya kutathimini maombi katika muda na maeneo yatakayobainishwa.

(6) Isipokuwa kwa wajumbe waliotajwa katika kanuni ndogo ya 2 (e) na (f), mjumbe anaweza kuwakilishwa endapo mjumbe huyo hatafika katika tarehe ambayo mkutano umepangwa.

Utoaji wa leseni

9.-(1) Mamlaka baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye kamati, itakuwa na mamlaka ya-

(a) kupitisha maombi na kutoa leseni kwa kipindi cha miaka mitatu;
(b) kurudisha maombi kwa mwombaji; au
(c) kukataa maombi.

(2) Bila kujali muda wa leseni uliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) (a), Mamlaka inaweza kutoa leseni ya muda mfupi kama mazingira yatahitaji hivyo na inaweza kumpa mwombaji leseni ya daraja husika kulingana na elimu na uzoefu wake bila kujali daraja la leseni aliloomba.

(3) Mwombaji aliyepewa leseni na Mamlaka,

ndani ya muda wa miezi mitatu, atachukua leseni yake kutoka kwa Mamlaka baada ya kulipa ada ya leseni kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(4) Bila kuathiri masharti yaliyopo katika Kanuni hizi, waombaji wa leseni maalum za kazi za matengenezo ya laini zenye umeme ni lazima wathibitishwe aidha na Taasisi yenye Ithibati au chombo kingine kinachotambulika na Mamlaka kinachofanya shughuli zinazoshabihiana.

(5) Leseni iliyotolewa chini ya kanuni hii itatumika na kumpa mamlaka mmiliki leseni kufanya kazi zake eneo la Tanzania Bara.

Kukataliwa leseni

10.-(1) Mamlaka inaweza kukataa kutoa leseni pale ambapo:

(a) Mamlaka imeridhika kwamba maombi hayakuzingatia masharti ya Sheria au sheria nyingine zinazotumika
(b) Mamlaka imeridhika kwamba mwombaji amewasilisha taarifa zaa uongo: na
(c) Mamlaka imeridhika kwamba mtu huyo kupewa leseni kutapelekea mgongano wa kimaslahi na mwajiri wake, na hili Mamlaka inaweza kuamua yenyewe au kwa kuombwa na mwajiri wa mtu huyo.

(2) Ikiwa Mamlaka itakataa maombi ya kutoa leseni, itamtaarifu mwombaji maamuzi hayo kwa maandishi, pamoja na sababu za maamuzi hayo.

U halali, muda na uhamishaji wa leseni

11.-(1) Mmiliki wa leseni atahifadhi leseni mahali salama kwa kipindi ambacho imetolewa na ikitokea imepotea au kuharibika, mmiliki wa leseni atapaswa kutoa taarifa mapema kwa Mamlaka na polisi kwa pamoja.

(2) Mamlaka baada ya kupokea taarifa ya kupoteza leseni na ada ya malipo yaliyoainishwa katika Jedwali la Tatu ya Kanuni hizi, inaweza kutoa nakala nyingine ya leseni.

Upandishaji daraja na uhuishaji leseni

12.-(1) Mmiliki wa leseni ambaye amepata sifa za juu katika kipindi cha leseni, zaidi ya daraja la leseni analomiliki, anaweza kuiomba Mamlaka kupandisha

leseni kwenda daraja husika la juu.

(2) Ikiwa mmiliki wa leseni ana nia ya kuhuisha leseni yake, atatuma maombi kwa Mamlaka miezi mitatu kabla ya muda wake kuisha.

(3) Mmiliki wa leseni ambaye ameshindwa kuomba kuhuisha leseni miezi mitatu baada ya leseni kuisha muda wake atapaswa kuomba leseni mpya.

Usitishaji na ufutaji leseni

13.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, Mamlaka inaweza kusitisha au kufuta leseni pale ambapo-

(a) Mamlaka imegundua kwamba leseni ilipatikana kwa kutoa taarifa au maelezo ya uongo kwa makusudi au uzembe;
(b) Mamlaka imegundua kwamba leseni ilipatikana kwa njia ya kughushi;
(c) mmiliki leseni amekiuka masharti ya Sheria, Kanuni hizi, au masharti na vigezo vya leseni;
(d) mmiliki leseni ambaye kwa makusudi au kwa uzembe amefunga mfumo wa umeme kwa kiwango duni; na
(e) mmiliki leseni amekutwa na hatia ya kosa linalohusiana na udanganyifu kuhusiana na leseni ya shughuli anazozifanya.

(2) Mamlaka kabla ya kusitisha au kufuta leseni chini ya kanuni ndogo ya (1), itampa taarifa ya maandishi mmiliki leseni ya nia ya kusitisha au kufuta leseni na itampa sababu ya kusitisha au kufuta na kumtaka mmiliki leseni kutoa maelezo ya sababu zitakazofanya leseni hiyo isisitishwe au isifutwe ndani ya siku thelathini.

(3) Mamlaka inaweza kusitisha au kufuta leseni, pale ambapo mmiliki wa leseni ameshindwa kutoa maelezo ya kuridhisha kwanini leseni hiyo isifutwe au isisitishwe.

(4) Baada ya leseni kusitishwa, Mamlaka itaeleza kwa maandishi, muda wa sitisho hilo.

(5) Baada ya kufuta leseni, Mamlaka itamtaarifu mmiliki wa leseni kwa maandishi kuhusu kufutwa kwa leseni na kwamba kutoka tarehe hiyo leseni iliyofutwa itakuwa batili.

(6) Mtu ambaye leseni yake imefutwa chini ya Kanuni hizi anaweza kuomba leseni mpya baada ya kupita muda wa miaka mitatu kutoka tarehe ya kufutwa leseni yake.

Kurudisha leseni

14.-(1) Mmiliki leseni ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea nakala ya amri ya kusitisha au kufutwa kwa leseni, anatakiwa kurudisha leseni kwa Mamlaka.

(2) Mtu ambaye anakiuka masharti ya kanuni hii atawajibika kulipa faini ya shilingi laki tano.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA MMILIKI LESENI

Kazi za ufungaji mifumo ya umeme

15.-(1) Mmiliki leseni atahakikisha kwamba kazi ya kufunga mifumo ya umeme, pamoja na nyongeza yoyote, mabadiliko na ukarabati kwenye mfumo uliopo hayafanyiki katika jengo lolote kwa niaba ya mteja, isipokuwa na mtu mwenye leseni ya kufunga mifumo ya umeme.

(2) Mmiliki leseni atahakikisha kwamba kazi zote za kufunga mifumo ya umeme zinafanyika katika Viwango vya Kitaifa vilivyopo au viwango vinavyokubalika katika tasnia ya umeme na sheria zinazohusika.

Uzingatiaji wa Sheria

16.-Mmiliki wa leseni, katika muda wa leseni, atazingatia:

(a) sheria zinazohusika, amri na maelekezo yanayotolewa na Mamlaka; na
(b) taratibu na viwango vya usalama, afya na mazingira.

Ukaguzi na majaribio

17.-(1) Mmiliki leseni atakagua, atafanya majaribio na ataandika taarifa ya ufungaji mfumo wa umeme ili kuhakikisha usalama wake.

(2)Mmiliki leseni kiongozi wa kufunga mfumo wa umeme, baada ya kumaliza kazi ya kufunga mfumo atahakikisha kwamba, nakala ya mchoro wa kufunga mfumo wa umeme unaandaliwa na kupewa mmiliki wa jengo kwa ajili ya kuhifadhi na mmiliki atahifadhi nakala hiyo na atapaswa kuonyesha pale ambapo Mamlaka itahitaji.

(3) Mmiliki leseni baada kumalizia kazi ya kufunga mfumo wa umeme, atatoa cheti kwa mteja katika muundo ulioainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi.

(4) Mamlaka inaweza, muda wowote, ikakagua jengo pale ambapo kazi ya ufungaji mfumo wa umeme imefanyika.

Ajali wakati wa ufungaji wa mfumo wa umeme

18.-(1) Mmiliki leseni atatakiwa kutoa taarifa mara moja kwenye Mamlaka pale ambapo ajali imetokea wakati wa kazi ya kufunga mfumo wa umeme ikiendelea.

(2) Mamlaka inaweza, pale inapoona kuna ulazima, kufanya uchunguzi kwa madhumuni ya kujua chanzo cha ajali ili kuwezesha Mamlaka kubainisha hatua za kuzuia kutokea tena kwa ajali na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

(3) Mamlaka inaweza, pale itakapoona kuna ulazima, kukodisha mtaalam wa kujitegemea kwa ajili ya kuchunguza tukio la ajali.

(4) Endapo ajali ni matokeo ya kutojali au uzembe wa mmiliki leseni na matokeo yake kusababisha madhara kwa mhanga wa ajali, mhanga anaweza kupeleka malalamiko kwenye Mamlaka kwa ajili ya fidia.

Wajibu wa mmiliki au mkazi katika jengo

19.-(1) Mmiliki au mkazi katika jengo atamtumia mtu mwenye leseni katika kufanya kazi ya ufungaji wa mfumo wa umeme.

(2) Mmiliki au mkazi katika jengo ambaye amekiuka kanuni ndogo ya (1), atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa faini ya shilingi milioni moja.

(3) Mmiliki au mkazi katika jengo atahakikisha mfumo wa umeme unakaguliwa na mtu mwenye leseni ya kufunga mfumo wa umeme kwa mujibu wa muda ulioainishwa katika Jedwali la Tano la Kanuni hizi.

(4) Mmiliki leseni, anapomaliza ukaguzi wa mara kwa mara, atatoa cheti kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Sita la Kanuni hizi.

(5) Endapo mmiliki wa jengo au mkazi amekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (3), jengo hilo litaonekana

halifai kusambaza umeme na pale ambapo Mamlaka itaona inafaa na kwa maslahi ya umma, inaweza kuteua mtaalam kufanya ukaguzi kwa gharama za mmiliki au mkazi.

## SEHEM U YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Makosa

20.-(1) Mmiliki leseni ambaye atafanya kazi ya kufunga mfumo wa umeme nje ya mipaka ya leseni yake atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi Laki Tano.

(2) Mmiliki leseni ambaye atafanya kazi yoyote ya kufunga mfumo wa umeme kinyume na Sheria na Kanuni hizi atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja.

Adhabu ya jumla

21. Mtu ambaye atakiuka masharti ya Kanuni hizi ambapo adhabu hazikuwekwa, atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu.

Adhabu kwa kuendelea kutenda kosa

22. Mtu yoyote ambaye anaendelea kukiuka masharti ya Kanuni hizi atawajibika kulipa faini ya shilingi laki moja kwa kila siku ambayo kosa linaendelea kutendeka.

Utoaji taarifa ya makosa

23.-(1) Endapo mtu amevunja masharti ya kifungu chochote ambacho faini imeainishwa chini ya Kanuni hizi, mtu huyo atatakiwa-

(a) pale ambapo anapinga kutenda kosa, kujaza Sehemu A ya Taarifa ya Kosa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Saba; au
(b) pale ambapo anakubali kutenda kosa, kujaza Sehemu B ya Taarifa ya Kosa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Saba.

(2) Endapo mtu anakubali kutenda kosa chini ya kanuni ndogo ya (1)(b), mtu huyo, ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya kukubali, atatakiwa kulipa faini iliyoainishwa.

Kukataa

24. Mtu yoyote ambaye amekataa kusaini Taarifa

kusaini Taarifa ya Makosa

ya Kosa pale anapohitajika na Mamlaka, atawajibika kulipa faini ya shilingi milioni tano.

Mamlaka ya kusimamia na taratibu za ziada

25. Mamlaka itasimamia Kanuni hizi kwa mamlaka iliyopewa chini ya Sheria, Sheria ya EWURA na Kanuni hizi.

Haki ya kukata rufaa

26. Mtu yoyote ambaye hataridhika na maamuzi ya Mamlaka chini ya Kanuni hizi anaweza kukata rufaa katika Baraza la Ushindani siku thelathini toka maamuzi kutolewa.

Kufutwa kwa T.S. Na. 404 of 2015

27.-(1) Kanuni za Umeme (Huduma ya Ufungaji Mifumo ya Umeme) ya mwaka 2015 imefutwa.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Kanuni za Umeme (Huduma ya Ufungaji Mifumo ya Umeme) za Mwaka 2015, amri zote, misamaha, au maelekezo yaliyotolewa au yanayosadikiwa kutolewa au yaliyotolewa chini ya Kanuni hizo yatachukuliwa kuwa yamefanyika chini ya Kanuni hizi, na yatabaki kuwa na nguvu kisheria mpaka pale itakapofutwa kwa rejea ya moja kwa moja au kuisha muda wake au kufikia ukomo wa kutumika.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

FAINI KWA KUFANYA KAZI ZA KUUNGANISHA UMEME BILA KUWA NA LESENI.

| NA. | Wigo wa eneo lililofanyiwa kazi bila leseni | Faini Inayopaswa kulipwa(TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Daraja“A” | 2,000,000.00 |
| 2 | Daraja“B” | 1,500,000.00 |
| 3 | Daraja “C” | 1,000,000.00 |
| 4 | Daraja“D” | 800,000.00 |
| 5 | Daraja “W” | 500,000.00 |
| 6 | Daraja “S1” | 2,000,000.00 |
| 7 | Daraja“S2” | 1,500,000.00 |
| 8 | Daraja“S3” | 1,000,000.00 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengezwa chini ya kanuni ya 5(2)(b))*

WASIFU WA WAOMBAJI WA LESENI YA KUUNGANISHA UMEME

SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO YA MWOMBAJI

<table>
<tr><td>1.</td><td colspan="3">Jina la Mwombaji: (Jina la Kwanza, Jina la Kati, Ukoo</td></tr>
<tr><td>2.</td><td colspan="3">Anuani ya Makazi:<br>Namba ya Kiwanja: ……........................................Namba ya Kitalu: ...........................................................<br>Mtaa: ......................................................................<br>Kata/Kijiji: ................................................<br>Miji/Jiji:.........................................................……<br>Msimbo wa Posta:.............................................................<br><br>Anuani ya Posta:<br><br>Sanduku la Posta:........................................... Mji/Jiji:................................ Msimbo wa Posta:......................……… Namba ya Simu.:..................................................Barua pepe:...................... ……. Namba ya Nukushi:.......................................<br>Simu ya mkononi:............................................</td></tr>
<tr><td>3.</td><td colspan="3">Taarifa Binafsi:<br>Tarehe ya Kuzaliwa:.............................Sehemu uliyozaliwa:...............................................<br>Jinsia(Ke/Me):.................<br>Utaifa:..............................<br>Hali ya Ndoa:............................Umri:…………………………<br>Kwa Mtu ambaye siyo raia<br>Jina la Mwombaji:……………………<br>Nchi uliyotoka……………Namba ya Pasipoti:..Tarehe iliyotolewa:................Tarehe ya kuisha muda wake:...................<br>Namba ya hati ya kufanya kazi.:....................Tarehe iliyotolewa:.........................Tarehe ya kuisha muda wake:............</td></tr>
<tr><td rowspan="5">4.</td><td colspan="3">Taarifa ya Ajira</td></tr>
<tr><td colspan="3">(anza na ya karibuni; fomu ya nyongeza inaweza kutumika kama nafasi haitoshi)</td></tr>
<tr><td colspan="2">Muda (mwezi,mwaka):</td><td rowspan="2">Ufafanuzi wa kazi yako, taja kazi ya kuunganisha umeme uliofanya, na eleza na kiasi cha msongo wa umeme .Pia, weka na majukumu yako/ mafanikio.</td></tr>
<tr><td></td><td></td></tr>
<tr><td>Mawasiliano:<br>Namba ya Simu ya mkononi:…………..</td><td></td><td></td></tr>
</table>

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Muda(mwezi,m w a k a ): | | | |
| | Kutoka……………… | | | |
| | Mpaka…………………. | | | |
| | Jina la Mwajiri na Anuani (kama umeajiriwa): | | | |
| | | | | |
| | Cheo Chako: | | | |
| | Jina la Msimamizi: | | | |
| | Mawasailiano:Namba ya simu ya mkononi: | | | |
| 5. | Barua pepe: | | | |
| | | | | |
| | Muda (Mwezi, Mwaka): | | | |
| | Kutoka……………… | | | |
| | Mpaka…………………. | | | |
| | Jina la Mwajiri na Anuani (kama umeajiriwa):: | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | Cheo Chako: | | | |
| | Jina la Msimamizi: | | | |
| | Mawasiliano:Namba ya simu ya mkononi: | | | |
| | Barua pepe: | | | |
| | Muda(Mwezi, M w a k a ): | | | |
| | Kutoka……………… | | | |
| | Mpaka…………………. | | | |
| | Jina la Mwajiri na Anuani ( Kama ni umeajiriwa) | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | Cheo Chako: | | | |

<table>
<tr><td></td><td colspan="2">Jina la Msimamizi:</td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Mawasiliano Simu ya Mkononi:…………Barua pepe:………..</td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td colspan="5">Taarifa ya Elimu:Kutoka juu kwenda chini:(Mafunzo ya Ufundi, chuo na Chuo Kikuu)</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Tarehe</td><td colspan="2" rowspan="2">Jina la Shule &Anuani</td><td rowspan="2">Cheti/Tuzo(Ambatisha cheti/tuzo kilichothibitishwa)</td></tr>
<tr><td></td><td>Kutoka</td><td>Mpaka</td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td colspan="2"></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td colspan="2"></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td colspan="2"></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td colspan="5">Mafuzo/kozi ulizosoma:</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Tarehe</td><td colspan="2" rowspan="2">Jina la Chuo& anuani</td><td rowspan="2">Cheti/Tuzo(Ambatisha cheti/ ushuhuda)</td></tr>
<tr><td></td><td>Kutoka</td><td>Mpaka</td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td colspan="2"></td><td></td></tr>
</table>

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td colspan="4">TAMKO:<br>Mimi natamka kwamba maelezo niliyoyatoa hapo juu ni ukweli kadri ya uelewa wangu.<br>Sehemu:………………………...<br>Jina:……………………….........<br>Tarehe:………………………..<br>Saini:…………………………</td></tr>
</table>

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya 5(2(e))*

ADA ZA LESENI

| Aina/Daraja la leseni | Ada ya mwaka ya kuhuisha leseni(TZS) | Ada ya mwanzo ya leseni | Ada za nakala za leseni |
|---|---|---|---|
| A,S1 | 100,000/- | 150,000 | 30,000 |
| B,S2 | 80,000/- | 120,000 | 25,000 |
| C,S3 | 60,000/- | 100,000 | 20,000 |
| D | 30,000/- | 60,000 | 15000 |
| W | 20,000/- | 40,000 | 10,000 |
| Maombi ya leseni | - | 10,000 | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 17 (3)*

Cheti cha Kumaliza Kazi ya Kufunga Mifumo ya Umeme

Cheti cha Kumaliza Kufunga Mifumo ya Umeme

Jina la mteja:……………………………………………………………

Eneo ambalo ufungajiumefanyika: Mtaa/Kijiji………………………………………………

Wilaya: ……………………………………………………....………………………………

Mkoa: ……………………………………………….………..…………………………..

Simu ya mkononi: ……………………………………………………………………………

Weka tiki (√ ) panapohusika

Aina ya majengo: Makazi ☐ Biashara ☐ Industrial ☐

Aina ya kazi ya uunganishaji unaofanyika: Mpya ☐ Uenezi ☐ Kubadilisha ☐

Nyingine (taja): ………………………………………..

Aina ya umeme unaosambazwa: njia moja ☐ usambazaji wa njia tatu ☐

Volti zinazosambazwa: 230 V ☐ 415V ☐ 11kV ☐ 33kV ☐ Zingine (taja) ……………

Kiasi kinachotazamiwa: …………………………………………………………………….

Tarehe ya kumaliza kufunga mifumo ya umeme………………………………..…………..

UTHIBITISHO
Mimi nathibitisha kwamba ufungaji wa mfumowa umeme ulioelezwa hapo juu umefanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kitaifa na ukaguzi wa kina kufanyika tayari kwa kuunganisha umeme.

Jina la Mmiliki Leseni: …………………………….
Saini: ……………………………………………….
Tarehe: ……………………………………………..

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19(3))*

VIPINDI VYA UKAGUZI WA UMEME

| AINA YA UFUNGAJI | MUDA WA KIPINDI CHA KUFANYA UKAGUZI (MIAKA) |
|---|---|
| Majengo ya Makazi | 5 |
| Majengo ya Viwanda | 3 |
| Majengo ya Biashara naHoteli | 2 |
| Majengo ya Hospitali | 5 |
| Majengo ya Shule/Vyuo | 5 |
| Sehemu za Burudani | 1 |
| Mfumo wa muda mfupi | 0.25 |
| Mahema/Makontena/Vibanda | 3 |
| Vibanda vya Mashine za kufua nguo | 1 |
| Sehemu za Maombi | 5 |
| Majengo ya Starehe | 1 |
| Majengo ya Umma | 5 |
| Vituo vya mafuta | 1 |
| Taa za dharura | 3 |
| Aina nyingine yoyote ya mifumo wa umeme usiotajwa hapa | 5 |

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19(4))*

Cheti cha Ukaguzi wa Kufunga Mifumo ya Umeme

Jina la Mteja:………………………………………………………

Eneo ulipo mfumo wa Umeme: …………………………………..

Wilaya: ……………………………………………………………

Dini: ………………………………………………………………

Simu ya Mkononi: ……………………………………………….

(weka tiki panapohusika)

Aina za Majengo: Makazi ☐ Biashara ☐ Kiwanda ☐

Aina ya umeme unaosambazwa: Njia moja ☐ Njia tatu ☐

Volteji zinazosambazwa: 230V ☐ 415V ☐ 11kV ☐ 83kV ☐ zingine (taja):……...

Kadirio la muda wa mfumo wa umeme unaofungwa: Miaka…………………

Tarehe ya mwisho wa ukaguzi: …………………………………………

Ushahidi wa Nyongeza au Mabadiliko: Ndiyo ☐ Hapana ☐ Isiyo dhahiri ☐

Taarifa zilizopo: Ndiyo ☐ Hapana ☐

TAMKO:

Mimi, nathibitisha kwamba mfumo wa umeme ambao taarifa zake zimetajwa hapo juu umekaguliwa na kujaribiwa kulingana na Viwango vya Kitaifa na kuthibitishwa kuwa hali yake inaridhisha/hairidhishi/inahitaji uangalizi wa haraka ili kuendelea na huduma.

Tarehe ya ukaguzi mwingine…………………………………….(kwa kujiridhisha).

Jina la Mmiliki Leseni: …………………………………………………

Namba ya Leseni: ……………………………………………..

Saini: ……………………………………………………………………

Tarehe: …………………………………………………………………….

JEDWALI LA SABA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 23)*

TAARIFA YA KOSA

Kwa..............................................................Anuani.................................................

1. Unashitakiwa kwa makosa yafuatayo:

(a) ........................................................................................................

(b).....................................................................................................

.(c)......................................................................................................

(d)......................................................................................................

(e) ………………………………………………..………………...

2. Endapo umekubali kutenda kosa unatakiwa kujaza “SEHEMU B” iliyopo chini na kutuma taarifa hii kwenye Mamlaka na kulipa adhabu iliyoainishwa kwa kila kosa ulilokubali ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe uliyopewa taarifa hii.

3. Endapo umekataa kutenda kosa unatakiwa kujaza “SEHEMU A” iliyopo chini na kutuma taarifa hii kwenye Mamlaka.

SEHEMU “A”-TAARIFA YA NIA YA KUJIBU MASHTAKA

Mimi..................................................….wa.....................................................(anuani) nikiwa mmiliki wa leseni, mkazi/mmiliki wa majengo, au …………………………………… nina nia ya kujibu kwenye Mamlaka /Mahakama katika shitaka Na. …………………………. lililoainishwa katika Aya ya 1 ya Taarifa hii.

Saini:...............................................

Tarehe:

SEHEMU “B”-KUKUBALI KOSA

Mimi...............................................................wa........................................ (anuani)nikiwa mmiliki wa leseni , mkazi/mmiliki wa majengo au ……………………………………. nakubali kutenda kosa Na……………………………………………. lililoainishwa katika Aya ya 1 ya Taarifa hii na nimeamua kulipa faini inayotakiwa ya kiasi cha TZS……………… ndani ya kipindi cha siku kumi na nne kutoka tarehe hii.

Signature:............................................... Tarehe:……............................................

Dodoma,
……………., 2021

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*